Swali la dola million: Je utakwenda mbinguni ukifa? Hili hapa jaribio la haraka. Je, umewahi kusema uongo, kuiba kitu chochote, au kulitaja bure jina la Mungu? Yesu alisema “Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Je, umewahi kuangalia kwa tamaa? Je, utakuwa na hatia siku ya Hukumu? Kama umefanya vitu hivyo, Mungu anakuona kama mwongo, mwizi, aliyekufuru na mzinzi katika moyo. Biblia inaonya kuwa ikiwa utakuwa na hatia utaishia Jehanamu. Mungu, ambaye Biblia inasema ni “mwingi wa rehema”, alimpeleka Mwanawe ateseke na kufa msalabani kwa ajili ya watenda dhambi wenye hatia. Tulivunja Sheria ya Mungu, lakini Yesu alilipa faini. Hii ina maana Mungu anaifuta kesi yetu kisheria kabisa. Anaweza kubadili hukumu yetu ya kifo, “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele”. Kisha Yesu akafufuka toka kwa wafu na kuyashinda mauti. Tafadhali tubu (geuka toka katika dhambi) leo na Mungu anawapa Uzima wa Milele kwa wote ambao wanaweka Imani yao katika Yesu Kristo. Kisha soma Biblia yako kila siku na uyatii maneno yake.

